Jina ______________________ Nambari ya usajili ______________
Shule ______________________ Tarehe ______________

Maagizo: Maswali ya kuchagua majibu — MUDA: SAA 1 DAK 40

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 1 hadi 10.**

Ulanguzi wa dawa za kulevya ni jambo linalopingwa na mataifa mengi duniani. Serikali za nchi mbalimbali zimekuwa macho **kuwabamba** wanaohusika na ulanguzi huu.

Katika jitihada hizi, wanaotoka na wanaoingia nchini huchunguzwa ili kuonekana kama wanasafirisha dawa za kulevya. Utafiti waonyesha kuwa, watu wengi wanaopatikana na hatia hii huadhibiwa vikali.

Dawa za kulevya zina madhara ambayo kila aliye na sikio angezingatia mafunzo dhidi yake. Kwa kufanya hivyo, watajitahidi kujiepusha nazo au kuziacha ikiwa wanahusika nazo.

Dawa hizi zimewafanya wengi kuwa mazuzu baada ya kuzitumia kwa muda mrefu kupita kiasi hata zikawadhuru akili zao.

Watoto wa watu wanaotumia dawa hizi huzaliwa wakiwa na kasoro fulani katika viungo vya mwili yao. Pia huwa na uzani mdogo.

Wakati mwingine, dawa hizi humfanya mtu asione vizuri, hivi kwamba macho huona vitu vidogo vikiwa vikubwa na vikubwa vikiwa vidogo. Kutoona huu, huwafanya madereva wanaotumia dawa hizi kusababisha ajali barabarani.

Maji yazidipo unga, watumiaji wa dawa hizi huipa dunia buriani. Kwa hivyo yafaa tujipe moyo na kushikana pamoja kupinga ulanguzi wa dawa za kulevya kwani, umoja ni nguvu utengano ni udhaifu na kwa pamoja tutashinda.

1. Ulanguzi wa dawa za kulevya unapingwa katika
   A. Kenya
   B. mataifa yote duniani
   C. mataifa mengi duniani
   D. serikali zote
2. Kulingana na habari hii,wanaochunguzwa ili kuzuia ulanguzi wa dawa hizi ni
   A. walevi
   B. madereva
   C. wasafiri
   D. kila mtu
3. Madhara ya dawa zinazozungumziwa ni yapi?
   A. Utapiamlo
   B. Watoto kuzaliwa wakiwa na kasoro mwilini na uzani mdogo
   C. Madereva huona barabara vizuri
   D. Kuyatumia kwa muda mrefu
4. Ni kwa nini madereva wanasababisha ajali?
   A. Hawaoni vizuri
   B. Hawasinzii
   C. Gari huendeshwa kwa kasi
   D. Huwa na njaa
5. Kuwabamba ni
   A. kuwashika na kuwaweka seli
   B. kupata ajali
   C. kudhurika
   D. kupigwa na polisi
6. Kufanya juu chini ni
   A. kwenda juu na chini
   B. kujitahidi kwa vyovyote vile
   C. kuwasaidia walio kwenye ngazi za juu na chini
   D. kuwasaka wahalifu

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

7. Methali ni ipi iliyotumika kwenye taarifa?
   A. Fanya juu chini
   B. Kwa udi na ambari
   C. Kutiwa mbaroni
   D. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu
8. Ili kuangamiza uhalifu huu, inafaa
   A. kunyamaza
   B. kuwahurumia wanaohusika
   C. kuungana na kupinga tabia hii
   D. kuwaadhibu wahusika
9. Ipi ni orodha ya dawa za kulevya?
   A. Chai, sigara na pombe
   B. Sigara, pombe na marijuana
   C. Miraa, kanabisi na kahawa
   D. Chai, kahawa na miraa
10. Kichwa bora kinachofaa habari hii ni
   A. Watoto wanaozaliwa na kasoro
   B. Vita dhidi ya madereva walevi
   C. Madhara ya dawa za kulevya
   D. Ajali za barabarani

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 11 hadi 20.**

Tunapenda kuwaarifu wakazi wote wa mtaa wa Majimoto kuwa kumekuwa na mlipuko wa ugonjwa wa kuambukiza katika maeneo ya karibu. Ugonjwa huu unasambaa kwa njia ya hewa, kugusana na majimaji ya mwili kutoka kwa mtu aliyeambukizwa. Dalili kuu za ugonjwa huu ni homa ya ghafla, kikohozi kikavu, maumivu ya misuli, uchovu mkubwa, na wakati mwingine, kuendesha au kutokwa vipele mwilini.

Kwa sasa, idara ya afya imechukua hatua za haraka kudhibiti maambukizi, lakini ni muhimu kila mmoja wetu kujikinga na kuchukua tahadhari zifuatazo: Nawa mikono kwa sabuni na maji safi yanayotiririka mara kwa mara. Epuka misongamano na kukaribiana sana na watu. Vaa barakoa hasa ukiwa kwenye maeneo yenye watu wengi. Jitahidi kuepuka kushika mdomo, pua na macho bila kunawa mikono. Kama una dalili zozote za kuvamiwa na maradhi hayo, tafadhali jitenge na uwasiliane na kituo cha afya kilicho karibu nawe.

Tafadhali sambaza ujumbe huu kwa wengine ili tupunguze kasi ya maambukizi. Afya yako ni jukumu lako!

Habari hizi zimetolewa na Idara ya Afya ya Mtaa
Tarehe: 12 Septemba, mwaka wa 2025.

11. Kifungu ulichokisoma kina lengo gani hasa?
   A. Kuwaeleza watu jinsi watakavyopata ugonjwa wa kuambukiza
   B. Kuwafahamisha watu kutoka Majimoto palipo na hatari
   C. Kuwapasha watu habari kuhusu maradhi ya kuambukiza
   D. Kusaidia watu kuepuka kuugua magonjwa ya kuambukiza.
12. Ili kujua kuwa mtu anaugua ugonjwa wa kuambukiza, mtu huyo huwa na yote haya isipokuwa
   A. kuwa na kikohozi kilichojaa majimaji na kamasi
   B. kuwa na vipele mwilini na tumbo la kuharisha
   C. kuwa na maumivu mengi kwenye mwili
   D. kupatwa na homa ya ghafla
13. Ni vigumu kupata ugonjwa huu kama
   A. maji ya mwili kutoka kwa anayeugua yamekufikia
   B. umemgusa na kumkaribia anayeugua
   C. hujamgusa wala kumkaribia anayeugua
   D. mnatumia hewa sawa na aliyeugua
14. Kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa kuambukiza ni jukumu la nani?
   A. Idara ya afya
   B. Serikali yetu
   C. Watu wazima na watoto
   D. Mtu binafsi
15. Ili kudhibiti maambukizi, mwandishi hajashauri kuwa
   A. waepuke palipo na umati mkubwa
   B. wazibe midomo au pua zao kwa mikono wakiwa kwenye watu wengi
   C. watu wanawe mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni
   D. kuhakikisha wanavaa barakoa wakiwa kwenye umati



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

16. Kama ni lazima mtu aguse sehemu za mwili kama pua au mdomo, ni lazima
A. avae barakoa
B. aondoke palipo na watu wengi
C. atafute ushauri wa daktari
D. anawe mikono kwa maji na sabuni

17. Mtu hujitenga au huwasiliana na kituo cha afya iwapo
A. amelemewa na dalili za ugonjwa huo
B. ameenda kwa watu wengi akiwa hajavaa barakoa
C. ameona ama kuhisi dalili ya ugonjwa
D. amekaribia mtu ambaye tayari ameambukizwa

18. Kasi ya maambukizi ni sawa na
A. mbio za maambukizi
B. dalili za maambukizi
C. madhara ya maambukizi
D. sababu za maambukizi

19. Neno sawa na ugonjwa ni ipi?
A. Sharubati
B. Ndwele
C. Zaraa
D. Adinasi

20. Kichwa kinachofaa habari hii ni
A. Ukosefu wa usalama
B. Uhalifu haulipi
C. Afya njema
D. Ugonjwa wa kuambukiza

**Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali 21 hadi 25.**

***(Marion na Neema wametoka shuleni jioni wakielekea nyumbani. Wanajadiliana barabarani kuhusu masomo ya shuleni mwao.)***

**Marion** : Siku hizi nimeanza kukichangamkia somo la Kiswahili zaidi ya kitambo. Kinanifurahisha sana. ***(Anapunguza kasi ya mwendo)***

**Neema** : Hunishindi. Kwanza tunapofunzwa kuhusu mavazi, mimi hufurahi na kuelewa

**Marion** : Tafadhali nikumbushe mwalimu alisema nini kuhusu mavazi jana, ***(Anajikuna kichwa)***

**Neema** : Hahaha! Marion, unasahau haraka sana. Mwalimu alisema kuwa kuna mavazi ya kike na kiume

**Marion** : ***(Huku akitabasamu)*** Naam, nakumbuka japo nakusihi unikumbushe vyema.

**Neema** : Kunayo mavazi ya kike na kiume. Mavazi ya kike ni kama vile gagro, shimizi........

**Marion** : Nashukuru sana kwa kunikumbusha.

21. Mazungumzo haya yanafanyika wapi?
A. Njiani
B. Sokoni
C. Nyumbani
D. Shuleni

22. Kati ya mavazi haya, ni vazi lipi huvaliwa na wanawake pekee?
A. Tai
B. Soksi
C. Sidiria
D. Kanzu

23. Kulingana na mazungumzo haya, ni wazi kuwa
A. wanafunzi hawa hawajivunii Kiswahili
B. wanafunzi hawa wanasoma shule tofauti
C. wanafunzi hawa hawapendi masomo
D. wanafunzi hawa wanakidhamini Kiswahili

24. Mazungumzo haya yanafanyika wakati gani?
A. Mchana
B. Adhuhuri
C. Jioni
D. Usiku

25. Mazungumzo haya ni baina ya watu wangapi?
A. Sita
B. Wawili
C. Wanne
D. Nane



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

**Soma kifungu kifuatacho. Kwa kila swali la 26 hadi la 40 , umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Hapo __26__ za kale katika kijiji cha Pondamali __27__ mtu __28__ na _29_ yake. Mtu ____30____ alikuwa ____31____ sana kwa staha aliyokuwa _32_. Aliwaheshimu watu wote wakubwa kwa wadogo wake ____33____ waume. Siku moja, alifanya ____34____ ____35____ liliwakera wanakijiji ____36____. Kioja ____37____ kilihusu __38____ ____39____ kijana wa kiume aliyewaachilia ngombe kuharibu mimea yake. Sifa y. ke ilichafuliwa zaidi ____40_____ kifungo cha maisha gerezani.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 26. | A. zamani | B. samani | C. zaidi | D. zamu |
| 27. | A. paliishi | B. palikua | C. palikuwa | D. paliisha |
| 28. | A. moja | B. mmoja | C. pamoja | D. kimoja |
| 29. | A. alaa | B. mwana | C. motto | D. aila |
| 30. | A. huo | B. huyo | C. huu | D. humo |
| 31. | A. akiheshimiwa | B. akiheshimu | C. akimheshimu | D. akiwaheshimu |
| 32. | A. naye | B. nao | C. nayo | D. nae |
| 33. | A. na | B. kuwa | C. kua | D. kwa |
| 34. | A. jambo | B. chambo | C. njabo | D. chambi |
| 35. | A. ambacho | B. ambalo | C. ambaye | D. ambayo |
| 36. | A. yote | B. wote | C. yoyote | D. wowote |
| 37. | A. wenyewe | B. chenyewe | C. lenyewe | D. yenyewe |
| 38. | A. maafu | B. maanga | C. maasi | D. mauaji |
| 39. | A. cha | B. ya | C. wa | D. la |
| 40. | A. alipohukumiwa | B. alihukumiwa | C. atahukumiwa | D. atahukumu |

**Kutoka swali la 41 hadi la 50, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.**

41. Andika sentensi hii kwa ukubwa
**Mto ule ni mpana**
A. Kijito kile ni kipana
B. Jito lile ni pana
C. Jito lile ni mapana
D. Mito ile ni mipana

42. Chagua kinyume kifaacho cha neno **vita**.
A. Imani B. Upendo
C. Kutopigana D. Amani

43. Ni nomino gani haipatikani katika ngeli ya **LI-YA**?
A. Goti B. Dawati
C. Kidole D. Godoro


44. Zifuatazo ni nomino za dhahania isipokuwa;
A. sukari B. mawaidha
C. maisha D. magonjwa

45. **Chagua wingi sahihi wa sentensi ifuatayo**
Nyani amekula ndizi iliyoiva
A. Nyani wamekula ndizi zilizoiva
B. Manyani wamekula ndizi zilizoiva
C. Nyani amekula ndizi zilizoiva
D. Manyani wamekula mandizi yaliyoiva

46. Kitenzi **'nawa'** katika kauli ya kutendesha ni
A. nawishwa B. nawika
C. nawisha D. navya

47. Sentensi, **'Amani ni ninga'** imetumia mbinu gani?
A. Tashbihi B. Tashhisi
C. Msemo D. Sitiari

48. Maumbo haya ni;



A. pia, pembe tatu pacha
B. mstatili, pembe tatu
C. moyo, pembe tatu pacha
D. kopa, pembe tatu

49. Bainisha matumizi ya maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi
Kikombe <u>hiki</u> ni changu, <u>kile</u> pale ni chako
A. Kivumishi, kiwakilishi
B. Kiashiria, kivumishi
C. Kielezi, kiwakilishi
D. Kiwakilishi, kivumishi

50. Chagua aina ya pambo ambalo huvaliwa miguuni:
A. Kikuku B. Kidani
C. Pete D. Kikuba



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com